

## TAHARIRI /WAZO/NUKUU/MSAMIATI

**Habarileo**  
Jumapili

## Usalama wa barabarani uanze na nidhamu ya dereva

**A**JALI za barabarani zimeendelea kuwa chanzo kikubwa cha vifo, majeraha na hasara za mali.

Pamoja na juhudi zinazofanywa na serikali kupitia vyombo vya usalama barabarani, bado baadhi ya madereva wameendelea kuendesha vyombo vya moto bila kuzingatia sheria na tahadhari muhimu.

Moja ya tabia hatari inayoongezeka na imekuwa ikichangia kwa kiasi kikubwa ajali za barabarani ni matumizi ya simu wakati wa kuendesha gari.

Hilo linathibitishwa na Mkuu wa kikosi cha Usalama Barabarani Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Boniface

Mbao aliyesema ajali nyingi za barabarani zinaendelea kutokea licha ya uwepo wa sheria na kanuni za usalama, kutokana na baadhi ya watumiaji wa barabara kushindwa kuzifuata ipasavyo ikiwa ni pamoja na kuendesha wakiwa wanatumia simu.

Alieleza kuwa matumizi ya simu wakati wa kuendesha gari ni moja ya sababu zinazochangia ajali kwani humfanya dereva kupoteza umakini na kushindwa kuwa mwangalifu.

Ni kweli matumizi ya simu yanapunguza unakini wa dereva kwa kiwango kikubwa sana.

Dereva kama binadamu huwa akifanya jambo anakuwa makini, hivyo anapokuwa

akizungumza, kutuma ujumbe au kutumia mitandao ya kijamii akiwa barabarani, macho na akili yake huondoka na kusababisha akose umakini barabarani.

Hali hiyo huongeza uwezekano wa kusababisha ajali ambazo mara nyingi zinaweza kuepukika kwa madereva kuwa makini zaidi.

Ni jambo la kusikitisha kuona baadhi ya madereva wakipuuza maisha yao na ya abiria na watumiaji wengine wa barabara kwa sababu ya simu.

Kitendo cha baadhi ya madereva kupokea simu badala ya kusimama pembeni, na wengine wakifanya hatari zaidi ya kufungua na kusoma ujumbe wakati wakiende-

sha na wanafikia hatua ya kuamua kujibu kabisa na ujumbe na kuutuma wakati wanaendesha magari.

Kitendo hicho ni ukiukwaji wa sheria za usalama barabarani na hakipaswi kuvumiliwa.

Rai yetu jamii ielewa kuwa usalama barabarani ni jukumu la kila mmoja.

Lakini pia madereva wanatakiwa kuweka mbele uhai wa watu kuliko mawasiliano ya simu ambayo yanaweza kusubiri.

Ni bora kuchelewa kujibu simu kuliko kusababisha ajali inayoweza kugharimu maisha, kusababisha majeraha au ulemavu wa kudumu maishani.

Tunaziomba pia mam-

laka husika kikiwemo kikosi cha usalama barabarani kuendelea kutoa elimu kwa madereva kuhusu madhara ya kutumia simu wanapopotesha.

Vilevile hatua kali zienelelee kuchukuliwa dhidi ya wanaokiuka sheria ili kutoa fundisho kwa wengine.

Kwa upande wa abiria nao wanapaswa kuwahimiza madereva kuzingatia usalama barabarani na kukemea matumizi ya simu wakati wa safari.

Ushirikiano wa pamoja utasaidia kupunguza ajali na kulinda maisha ya Watanzania.

Imani yetu ajali za barabarani zinaweza kuepukika iwapo watumiaji wote wa

barabara na vyombo vya moto watashirikiana kwa kukumbushana wajibu, misingi, kanuni na sheria za barabarani.

Abiria ukisema siyo kazi yangu kumkemea dereva unapooona anaendesha gari bila kuzingatia sheria, mwisho wa siku inapotokea ajali ndiyo mnakemea haina maana yoyote kwa sababu tayari athari imetokea kama siyo kifo, basi majeraha au ulemavu.

Tunawasihani na kuwakumbusha madereva kila mmoja kuwa makini akiwa barabarani.

Epukeni kutumia simu wakati wa kuendesha ili kulinda maisha yenu na ya wengine. Usalama kwanza, simu baadaye.

**Wakimbizi ni ndugu zetu,**